

JINA LA RIWAYA: DARAJA LA MAUTI

MWANDISHI: MWARABU OMARI

NAMBARI YA SIMU: +254793743469

...anaonekana amerudi tena kule makaburini. Kasimama mkabala ya makaburi matatu yaliyorembwa kwa vigae vya rangi ya dhahabu vyenye nakshi ya kiimarati. Moyoni, fundo la uchungu limemsakama lakini hana budi kuogelea kwenye bahari hio kwani aliyavulia nguo mwenyewe. Anajaribu kuituma akili yake kwengine ili asiweze kukumbuka yaliyojiri hasa hadi saa hii akawa mahali hapa.

Kaburi la kwanza lilikuwa limeandikwa bwana Heri Japai na picha yake imetundikwa chini ya jina hilo. La pili limeandikwa bi Raufu Japai na la tatu Mwene Heri Japai huku picha zao zote zimetundikwa mtawalia. Je, kwani majina haya yana msuko gani na Japai. Je, ni watoto wake kwa jinsi majina yao yalivyo ama? Na kwanini aweze kuzuru makaburi haya? Japai anaonekana mwangi wa mawazo. Anatatarika huku na kule kama kuku anaetaka kutaga. Kupitia mawazo yake yaliyotokosa ubongo wake na kuufanya kuwa rojorojo ndipo tunajua kuwa makaburi hayo ni ya babake, mamake na dadake. Kuna kitu fulani kila akikumbuka anaonekana kutokwa ni machozi. Mara kwa mara anajifuta machozi kwa hankachifu yake.

Kwenye upeo wa akili yake anaona sura ya babake ikisemezana naye. "Mwanangu ulishikwa ni ibilisi gani hadi ukafanya hivi? Umepata faida gani kwa hili? Angalia mikono

yangu , umeifunga silisili!! Hakika wewe si damu yangu.”

Mara anamuona mama yake akiokota kuni. Baada ya kuokota akazifunga rita na kuzibeba. Kila anapoendelea na safari yake anaongeza kuni licha ya kuwa rita linazidi kuwa zito sana hadi anatataga. Badala ya kupunguza kuni, ye bado angali kuendelea kuongeza kuni. Taswira ya mwisho anayoionna upenuni mwake ni ya dadake kipenzi Mwene. Mwene yumo katikati ya bwawa la damu huku akiwa amefungwa minyororo. Analia kwa uchungu sana. “Kaka, kwanini uamue kunitesa hivi, kwanini?” hapo Japai akaamua atoe mawazo yake upenuni kwani yalikuwa yakimletea majonzi tu na si chengine. Aidha alirusha fikra na kuirudisha miaka arobaini nyuma, wakati alipokuwa mtoto.

Babake alikuwa akipenda kumbeba mabegani kwake kila mara. Si hayo tu, bali pia alikuwa akiadhibiwa na kuonywa vikali pindi akikosa. Pia anakumbuka jinsi mama yake alivyokua akimtetea kwa watoto wengine hata kama kafanya kosa. Ilmradi tu mama ni mama hata awe aina gani, awe mrefu au mfupi, mweupe au mweusi, mnene au mwembamba. Ala kulihal yeye ni mama. Hapo Japai alijichorovy a machozi na kulowesha kifua chake huku akiupiga darubini utajiri wake. Anajiuliza kimoyomoyo, je utajiri ulionao Japai una maana zaidi ya wafu watatu walio mbele ya haki? Lakini afanyeje? Kinachobaki rohoni mwake ni kusema tu, laiti ningelijua. Lakini je, yote haya yalianza vipi?...